# Mpiga Risasi Hai na Zuio la Kutoka Nje

Anzisha sera ya maandishi kuhusu kujitayarisha na majanga ili kujumuisha vitisho vya ndani na nje na shughuli za uhalifu. Taratibu za zuio la kutoka nje zinapaswa kuzingatia mpangilio maalum wa vifaa na muundo kwenye kituo. Jitayarishe, panga na ufanye mazoezi.

## Mpango

- Bainisha chumba/vyumba katika jengo ambacho/ambavyo kinaweza/vinaweza kutumika kama chumba/vyumba salama iwapo tahadhari ya kutotoka nje au amri ya kutoka ikitolewa.
- Hakikisha kuwa kina mlango mgumu wa chuma wenye kufuli madhubuti.
- Hakikisha kina simu au njia nyingine za mawasiliano.
- Hakikisha chumba kina chakula cha kutosha, maji, seti au vifaa vya huduma ya kwanza ya kiwewe (ikiwemo tourniquet, vitambaa vya kuziba majeraha) na vilevile choo au choo cha watu wenye ulemavu wa viungo.
- Zingatia kujumuisha vitu vya ziada vinavyoweza kutumika kukinga mlango (yaani kamba au ukanda kwa utaratibu wa kujifunga).
- Anzisha eneo la kukimbilia nje ya kituo iwapo dharura itatokea.

## Jiandae

- Wape majukumu wafanyikazi wakati wa hali ya zuio la kutoka nje, ikiwemo:
  - Kufunga kwa ufunguo milango ya nje.
  - Kufunga milango ya ndani ili kuongeza vizuizi.
  - Fagia kituo na uwaelekeze watu kwenye chumba cha zuio la kutoka nje.
  - Fikiria kazi maalum za ziada.
- Tunza kiendeshi cha USB au faili yenye ramani au michoro ya jengo, orodha ya wafanyikazi, na maelezo ya janga lililotokea kwenye kituo, n.k. kwa ajili ya utekelezaji wa sheria.
- Mtambue mtu atakayetumika kama mtu wa kuwasiliana naye kwa ajili ya utekelezaji wa sheria.
- Fanya mazoezi ya zuio la kutoka nje na uokoaji wa dharura kwa mara nyingi.

# Mpiga Risasi Hai – Yajue machaguo yako

Matukio hai ya shambulio hayatabiriki na yanaweza kubadilika; waathiriwa huchaguliwa kwa nasibu. Mshambuliaji huchagua maeneo yenye watu wengi na/au yaliyozuiliwa ili kuua au kujeruhi watu wengi kadri iwezekanavyo. Jua na uelewe machaguo yako.

### Kimbia

- Jua njia yako ya kutorokea.
- Acha vitu vyako.
- Ondoka bila kujali kama wengine wanakufuata.
- Waonye wengine na uwazuie kuingia.
- Piga simu 911 unapokuwa salama.

### Jifiche

- Hakikisha hauonekani kabisa.
- Funga na uweke kizuizi mlangoni.
- Zima taa.
- Zima sauti ya simu yako.

### Pambana

- Pambana kama suluhu la mwisho tu pale ambapo maisha yako yapo hatarini.
- Tupa vitu, tafuta silaha.
- Fanya fujo za mwili kadri iwezekanavyo, maisha yako yanategemea hilo.

## Maafisa wa Kutekeleza Sheria Wanapokuwa Wamefika

- Maafisa wa awali kwenye eneo la tukio wataelekea moja kwa moja kwenye tishio; timu za uokoaji zitafuata.
- Fuata maelekezo yote ya vyombo vya utekelezaji wa sheria.
- Nyosha mikono yako juu.
- Usiwafuate haraka maafisa; epuka kupiga kelele, kupiga yowe na kunyosha kidole.
- Usiulize maswali wakati unatoroka.

**Nyenzo za Ziada: https://www.dhs.gov/cisa/private-citizen**